



Kitengo Cha Lugha Nyingi, EFF

- Ufundishaji wa Lugha Mama kwenye shule za msingi, shule za msingi maalum, shule za sekondari na shule za sekondari maalum
- Usaidizi kwa kutumia Lugha Mama kwenye masomo mengine
- Usaidizi kwa utangulizi/utambulisho kwa Lugha Mama
- Kufanya utafiti kwa kutumia Lugha Mama
- Mtihani wa somo au kozi ya Lugha Mama

Enheten för flerspråkighet

flersprakighet@uppsala.se

018-727 20 26



Modersmålsundervisning



flersprakighet.uppsala.se



Nani anastahili somo la Lugha Mama?

(OBS Hii haitumiki kwa Lugha za wachache wa kitaifa)

Mwanafunzi ambaye Kiswidi si Lugha Mama ya mlezi wake, anapewa nafasi ya kujifunza Lugha Mama kama:

1. *Lugha Mama ya mwanafunzi inatumika kila siku nyumbani na,*
2. *Mwanafunzi ana ujuzi wa msingi wa lugha hiyo.*

Mwanafunzi awe anasema na kuelewa lugha. Somo linafundishwa kwa Lugha Mama kwa kufuata mtaala wa taifa.

Lugha za wachache wa kitaifa

Lugha za wachache Uswidi ni: KIFINI, KIMEÄNKELI, KISAMI, KIROMANI na KIYIDI. Ili kujifunza mojawapo ya lugha hizi, lazima uwe mzaliwa wa wasemaji wa lugha hizi. Mwanafunzi hahitaji kusema lugha hiyo nyumbani au kuwa na ujuzi wa msingi. Mwanafunzi anapojaza fomu ya maombi, anachagua kati ya msemaji wa lugha hiyo au kama ataanza kujifunza upya.

Kitengo cha Lugha Nyingi (EFF) kinaratibu ufundishaji wa Lugha Mama Uppsala.

Ujuzi wa msingi

Ujuzi wa msingi unahitajika kwa lugha zote isipokuwa kwa lugha za wachache. Mwalimu anatathmini ujuzi wa msingi wa mwanafunzi wakati kozi inapoanza. Ufahamu wa kusikia na uwezo wa kusema hupimwa. Maelezo kuhusu ujuzi wa msingi yanapatikana kwenye tovuti (website) ya EFF.

Kutuma maombi

Mlezi wa mwanafunzi ndiye anayetuma maombi. Fomu za maombi zinapatikana shuleni na kwenye website ya EFF. Jaza fomu hiyo, weka sahihi na uipeleke kwenye shule ya mwanafunzi. Mwalimu mkuu anapitisha maombi na kuyatuma EFF kabla ya juni 15 tayari kwa muhula unaofuata. Maombi baada ya juni 15 hayana uhakika wa kupatiwa nafasi.

Mpangilio wa ufundishaji

Uppsala imetoa fursa ya ufundishaji wa Lugha Mama baada ya saa za masomo. Muda wa ufundishaji wa Lugha Mama hupangwa baada ya masomo ya siku. Shule za awali hadi darasa la tano hufundishwa mashuleni pao. Darasa la 6–9 huekwa kwenye vikundi na hupangiwa shule wanapokutana wakati wa alasiri au jioni. Wanafunzi huenda wenyewe shuleni na wale wanaohitaji usafiri hupewa tikiti za basi na mwalimu wao wa Lugha Mama.

Habari zaidi

Kwenye website ya EFF utapata habari zaidi za ufundishaji wa Lugha Mama Uppsala.

flersprakighet.uppsala.se

